# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Telegrams: "UTUMISHI", DAR ES SALAAM
Tel. No. : +(255) 22 2118531-4
Fax No.: +(255) 22 2125299
E-mail: permsec@utumishi.go.tz

OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA,
JENGO LA UTUMISHI,
8 BARABARA YA KIVUKONI,
S.L.P. 2483,
11404 DAR ES SALAAM.

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na. EG. 45/86/01/"D"/** 48 07 Oktoba, 2015

Makatibu Wakuu Wote,
Wakuu wa Idara Zinazojitegemea Wote,
Watendaji Wakuu wa Wakala za Serikali Wote,
Makatibu Tawala wa Mikoa Wote,
Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa na Miji Wote,
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya Wote.

**YAH: UTEKELEZAJI WA AHADI YA UADILIFU KWA WATUMISHI WA UMMA**

Tafadhali rejea somo hilo hapo juu.

2. Pamoja na barua hii, nawasilisha kwenu Nakala ya *Fomu ya Ahadi ya Uadilifu kwa Watumishi wa Umma* pamoja na Nakala ya *Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.2 wa mwaka 2015* kuhusu utekelezaji wa ujazaji wa Fomu ya Ahadi ya Uadilifu kwa Watumishi wa Umma. Nakala za Fomu ya Ahadi ya Uadilifu na Waraka tajwa zinapatikana kupitia Tovuti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma – www.utumishi.go.tz. Utaratibu wa kukutumia Nakala ngumu (hard copy) unaandaliwa na Ofisi yangu kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi.

3. Ili kutekeleza suala hili kwa ukamilifu, Waajiri wanashauriwa kutenga muda au siku maalum ya kutekeleza agizo hili, kuwawezesha watumishi katika makundi tofauti kupata fursa ya kupitia kwa pamoja maelezo yaliyomo katika fomu hii ya Ahadi ya Uadilifu na kisha kusaini. Baada ya kusaini, nakala moja atakabidhiwa Mtumishi na nakala nyingine itawekwa kwenye jalada lake binafsi. Zoezi hili litaendelea kufanyika kila mwaka kwa watumishi wa Umma wote.

4. Ni jukumu la Wizara, Ofisi na Taasisi nyingine kuhakikisha kuwa Taasisi na Ofisi zote zilizopo chini yake zinatekeleza agizo hili kwa ukamilifu. Pia mnatakiwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa suala hili mwezi Juni

kila mwaka ili kuiwezesha Ofisi yangu kuratibu utekelezaji wa agizo hili kama ilivyoelekezwa katika Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa mwaka 2015 aya ya 4(4.1)(b) na 7.

5. Tafadhali mnaombwa kukiri kupokea barua hii ili kuweka kumbukumbu sahihi.

Nawashukuru kwa ushirikiano wenu.

HAB Mkwizu
**KAIMU KATIBU MKUU (UTUMISHI)**

Nakala: 1. Katibu Mkuu Kiongozi,
Ofisi ya Rais - IKULU,
S.L.P 9120,
**DAR ES SALAAM.**

2. Kamishna,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma,
Mtaa wa Ohio,
S.L.P 1334,
**DAR ES SALAAM.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Telegrams "CABINET"
DAR ES SALAAM
Simu Na: 2116898, 2116900/6
Barua pepe: chief@ikulu.go.tz
Barua pepe: ikulu@ikulu.go.tz
Fax: 2113425/2116914/2117272
Unapojibu tafadhali taja:

OFISI YA RAIS
IKULU,
1 BARABARA YA BARACK OBAMA
11400 DAR ES SALAAM

Kumb. Na. CAB 157/433/1/27

01 Agosti, 2015

# WARAKA WA MKUU WA UTUMISHI WA UMMA NA. 2 WA MWAKA 2015

## KUHUSU UTEKELEZAJI WA AHADI YA UADILIFU KWA VIONGOZI, WATUMISHI WA UMMA NA SEKTA BINAFSI

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 Misingi ya maadili nchini ina historia ya siku nyingi ambapo baada ya Uhuru, kuliwekwa ahadi zilizosaidia kuhamasisha wananchi kujenga ari ya uzalendo, uadilifu, na kuchukia rushwa na unyonyaji. Misingi hii iliwaongoza wananchi katika kufikia malengo yao ya maendeleo. Baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini mwaka 1992, ahadi hizo hazikupewa msukumo mkubwa kutokana na kuhusishwa na mfumo wa chama kimoja cha siasa.

1.2 Ili kuziba pengo hilo, ilitungwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, sura ya 398, ili kuweka misingi ya kisheria kuhusu maadili ya uongozi na utumishi wa umma. Aidha, Serikali iliunda Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi ambayo, pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sheria hii, ilipewa pia jukumu la kukuza maadili ya uongozi nchini.

1.3 Kwa kuwa maadili ni jambo mtambuka linalowahusu wananchi wote, Serikali pamoja na hatua nyingine, iliunda vyombo mbalimbali vya kueneza na kuimarisha maadili ya Viongozi na Watumishi wa Umma, pamoja na wananchi kwa ujumla. Hatua hizo ni pamoja na kuhuishwa kwa Kanuni za Maadili ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma za mwaka 2005, na kutungwa upya kwa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007. Aidha, Serikali pia imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

1.4 Pamoja na juhudi hizi, upo umuhimu wa kuendelea kubuni mikakati mingine na kuimarisha mikakati iliyopo. Hivyo, Serikali imeanzisha utaratibu wa kuhamasisha uadilifu kwa Viongozi, Watumishi wa Umma na Sekta Binafsi kupitia Ahadi za Uadilifu (*Integrity Pledges*).

## 2.0 MADHUMUNI YA WARAKA

Madhumuni ya Waraka huu ni kuweka utaratibu wa utekelezaji wa Ahadi za Uadilifu kwa Viongozi na Watumishi wa Umma na wale wa Sekta Binafsi. Waraka huu unawahamasisha kuwa waadilifu, wawazi, wawajibikaji, wenye kuzingatia weledi katika kuhudumia umma. Waraka pia unahimiza ari ya kupambana na rushwa na maovu mengine, pamoja na kuwashirikisha wananchi katika kufuatilia ukiukwaji wa maadili miongoni mwa Viongozi, Watumishi wa Umma na Sekta Binafsi na kutoa taarifa kwa mamlaka husika.

## 3.0 MISINGI YA WARAKA

3.1 Ahadi ya Uadilifu ni tamko rasmi na bayana la dhamira ya kuwa mwadilifu na kuunga mkono Kampeni ya Kitaifa kuhusu Maadili na Mapambano dhidi ya Rushwa. Ahadi ya Uadilifu ni tamko la dhamira ya uongozi na watumishi kwenye sekta ya umma na ya binafsi kuzingatia kanuni za maadili ya umma.

3.2 Pamoja na kuwepo Sheria, Kanuni, Miongozo na Mikakati ya Kukuza Maadili na Kupambana na Rushwa, bado rushwa ipo na lazima iendelee kupigwa vita. Wananchi nao wameendelea kusumbuliwa na urasimu usio wa lazima na utoaji wa huduma usioridhisha unaotengeneza mazingira ya rushwa.

3.3 Kwa upande mwingine, huko nyuma, sekta binafsi haikushirikishwa vya kutosha katika Mkakati wa Kupambana na Rushwa. Rushwa inaonekana ni tatizo la sekta za umma wakati ambapo wanaotoa na kupokea rushwa wako pia katika sekta binafsi. Hivyo Sheria, Kanuni, Miongozo na Mikakati iliyopo haiwezi peke yake kupunguza au kumaliza kabisa tatizo la rushwa na utovu wa maadili nchini. Lazima wadau wote washirikishwe na wakaribishwe kutoa Ahadi ya Uadilifu. Hii ni fursa kwa Sekta Binafsi kuonesha utayari wao kushiriki mapambano haya.

## 4.0 UTEKELEZAJI WA AHADI YA UADILIFU

4.1 Utekelezaji wa Ahadi ya Uadilifu utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma itasimamia utekelezaji wa jumla wa Ahadi ya Uadilifu kwa Viongozi wa Umma na kutoa Hati ya Ahadi ya Uadilifu kwa Viongozi wa Umma;

(b) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaratibu utekelezaji wa Ahadi ya Uadilifu na kutoa Hati ya Ahadi ya Uadilifu kwa Watumishi wa Umma kwa kuwashirikisha Watendaji Wakuu wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Wakala za Serikali, Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(c) Wakala ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) itasimamia utekelezaji wa Ahadi ya Uadilifu na kutoa Hati ya Ahadi ya Uadilifu kwa makampuni binafsi.

4.2 Sekretarieti ya Maadili na Mamlaka zilizotajwa zina wajibu wa kuandaa orodha ya Viongozi, Watumishi wa Umma na Makampuni yanayotakiwa kusaini Ahadi ya Uadilifu.

4.3 Kamishna wa Maadili, Watendaji Wakuu wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na Mtendaji Mkuu wa BRELA, wataweka saini Hati hizo kama wasimamizi wa utekelezaji, kila mmoja kwa mamlaka aliyonayo.

4.4 Kutokana na maelekezo haya, Viongozi wote wa Umma waliotajwa katika Sheria ya Maadili ya Viongozi, Watumishi wote wa Umma, na Makampuni yaliyosajiliwa Tanzania, yatapaswa Kujaza Hati ya Ahadi ya Uadilifu na kuwasilisha kwa Mamlaka inayohusika. Aidha, wahusika wanapaswa kushiriki kikamilifu katika Kampeni ya Kitaifa ya kuhamasisha maadili na elimu kuhusu umuhimu wa Ahadi ya Uadilifu katika mapambano dhidi ya rushwa na utovu wa maadili.

4.5 Mamlaka zote za ajira zinaelekezwa kuhakikisha kuwa Ahadi ya Uadilifu inakuwa sehemu ya barua ya ajira na uteuzi wa Viongozi na Watumishi wa Umma kama zilivyoambatishwa na Waraka huu.

5.0 WANAOHUSIKA NA WARAKA

Waraka huu unawahusu Viongozi na Watumishi wote wa Umma katika Utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Makampuni Binafsi yanayoendesha shughuli zake ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

6. MATARAJIO YA UTEKELEZAJI WA WARAKA

Inategemewa kuwa, utekelezaji wa Waraka huu utajenga mwitikio na dhamira ya uadilifu, uwazi, uwajibikaji, ari ya kupambana na rushwa na utoaji wa huduma bora katika Sekta ya Umma na Binafsi.

7. UTEKELEZAJI WA WARAKA

7.1 Usimamizi na utekelezaji wa Waraka huu utakuwa kama ilivyofafanuliwa katika aya ya 4 ya waraka kuhusu Utekelezaji wa Ahadi za Uadilifu.

7.2. Waraka huu unaanza kutumika leo tarehe 01 Agosti, 2015.

*Balozi* Ombeni Y. Sefue
KATIBU MKUU KIONGOZI NA
MKUU WA UTUMISHI WA UMMA

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA
## AHADI YA UADILIFU KWA WATUMISHI WA UMMA
## *(Kwa Utumishi wa Umma uliotukuka)*

Kwa kutambua dhamira ya kuufanya utumishi wa umma kuwa wenye ufanisi na kuheshimika kutokana na watumishi kufuata Sheria ya Utumishi wa Umma, Na. 8 ya mwaka 2002, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 na Kanuni za Maadili ya Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma za mwaka 2005 pamoja na kuwa na mwenendo unaozingatia maadili; Mimi........................................................ ninaahidi kwa umma kwamba:

1. Nitakuwa Mzalendo kwa nchi yangu na mtii kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
2. Nitahudumia umma na watumishi wenzangu kwa heshima;
3. Nitatimiza wajibu wangu wa kutoa huduma bora kwa umma;
4. Nitatoa huduma bora kwa usawa kwa watu wote na kutofanya ubaguzi kwa misingi ya dini, siasa, kabila, udugu, ukanda, jinsia, urafiki au hali ya mtu;
5. Sitaomba, kushawishi, kutoa wala kupokea rushwa;
6. Sitaomba, kutoa wala kupokea zawadi au fadhila za kiuchumi au za kisiasa au kijamii zisizoruhusiwa na Sheria;
7. Sitatumia madaraka yangu kwa manufaa binafsi, ya ndugu, rafiki au jamaa zangu;
8. Nitatekeleza wajibu wangu kwa kufuata Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbali mbali ya Utumishi wa Umma;
9. Nitafanya kazi kwa bidii na nidhamu ya hali ya juu;
10. Nitalinda na kutumia rasilimali za umma kwa manufaa ya umma;
11. Nitaepuka tabia ambayo inavunja heshima ya utumishi wa umma hata ninapokuwa nje ya mahali pa kazi;
12. Sitatoa siri za Serikali au za mteja kwa watu wasiohusika isipokuwa kwa maslahi ya umma;
13. Nitajiepusha na mgongano wa maslahi na pale utakapojitokeza nitaututatua kwa maslahi ya umma.

**Tamko:** Ninakiri kwamba nimeisoma Hati hii ya Ahadi ya Uadilifu kabla ya kuweka sahihi. Ninakubaliana na kutambua kwamba masharti yaliyo katika Hati hii ni ya kimaadili na kisheria na ninawajibika kuyatekeleza. Ninaelewa kwamba ukiukwaji wa masharti hayo ni ukiukwaji wa maadili na masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sheria ya Kudhibiti Mgongano wa Maslahi, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma, Kanuni za Maadili ya Kitaaluma na kwamba hatua za kinidhamu na kisheria zinaweza kuchukuliwa dhidi yangu iwapo nitakiuka masharti hayo.

| ............................ | ........................ | .................. | .................. |
| --- | --- | --- | --- |
| **JINA** | **CHEO** | **SAINI** | **TAREHE** |

| ................................................ | ................ | .................. | .................. |
| --- | --- | --- | --- |
| **MTENDAJI MKUU WA TAASISI** | **TAASISI** | **SAINI** | **TAREHE** |